# PRIVACY NOTICE

# TAARIFA YA FARAGHA

JUSTDIGGIT

Your privacy matters to us. In this Privacy Notice (**Privacy Notice**) we explain how Stichting Justdiggit Foundation (**Justdiggit** or **we**) uses your personal data we collect through our Kijani App (**Kijani App**).

Faragha yako ni muhimu sana kwetu. Katika Taarifa hii ya Faragha (**Taarifa ya Faragha**) tumeeleza namna Shirika la *Stichting Justdiggit* (**Justdiggit** au **sisi**) linavyotumia taarifa zako binafsi ambazo hukusanywa kupitia Aplikesheni yetu ya Kijani (**Aplikesheni ya Kijani**).

We are committed to protecting your privacy and ensuring the security of your personal data. Please read this Privacy Notice carefully to understand our practices regarding your personal data and how we will treat it.

Tumejizatiti kulinda faragha yako na kuhakikisha usalama wa taarifa zako binafsi. Tafadhali soma Taarifa hii ya Faragha kwa makini ili uelewe namna tunavyozitumia taarifa zako binafsi na jinsi tunavyozishughulikia.

**This Privacy Notice explains the following:**

**Taarifa hii ya Faragha inafafanua yafuatayo:**


1 WHO IS THE DATA CONTROLLER? 1

*NANI ANADHIBITI TAARIFA?*

2 HOW DO WE COLLECT YOUR PERSONAL DATA? 1

*TUNAKUSANYAJE TAARIFA ZAKO BINAFSI?*

3 THE TYPES OF PERSONAL DATA WE COLLECT FOR OUR PURPOSES AND THE APPLICABLE LEGAL BASIS FOR OUR DATA PROCESSING? 2

AINA YA TAARIFA BINAFSI TUNAZOZIKUSANYA KWA MATUMIZI YETU PAMOJA NA MSINGI WA KISHERIA UNAOTUMIKA KATIKA UCHAKATAJI WETU WA TAARIFA

4 HOW LONG DO WE RETAIN YOUR PERSONAL DATA? 3

JE, TAARIFA ZAKO BINAFSI TUNAZIHIFADHI KWA MUDA GANI?

5 WITH WHOM WE SHARE THE PERSONAL DATA? 3

JE, TAARIFA ZAKO BINAFSI TUNAZITUMIA NA NANI?

6 WHERE DO WE STORE YOUR PERSONAL DATA? 4

JE, TAARIFA ZAKO BINAFSI TUNAZIHIFADHI WAPI?

7 YOUR RIGHTS 4

HAKI ZAKO

8 RIGHT TO LODGE A COMPLAINT 5

HAKI YA KUWASILISHA MALALAMIKO

9 CHANGES TO THIS PRIVACY NOTICE 5

MABADILIKO YA TAARIFA YA FARAGHA

## 1 WHO IS THE DATA CONTROLLER?

### NANI ANADHIBITI TAARIFA?

Your personal data is collected by Justdiggit. Our registered office is at Prins Hendrikkade 25, 1012 TM Amsterdam. You can contact us via email at info@justdiggit.org or by telephone at +31 (0)20 737 23 66. Additionally, the Kijani App provides a functionality that allows you to contact us via Whatsapp. We are the data controller under the General Data Protection Regulation (**GDPR**), responsible for deciding how and why your personal data is used.

Taarifa zako binafsi zinakusanywa na Justdiggit. Ofisi yetu iliyosajiliwa iko Prins Hendrikkade 25, 1012 TM Amsterdam. Unaweza kuwasiliana nasi kwa njia ya baruapepe info@justdiggit.org au kwa simu +31 (0) 20 737 23 66. Vilevile, Aplikesheni ya Kijani inakuwezesha kuwasiliana nasi kwa njia ya WhatsApp. Sisi ni wadhibiti wa taarifa chini ya Sheria Majumui za Ulinzi wa Taarifa (**GDPR**), tunashughulika na kuamua namna na sababu za kutumika kwa taarifa zako binafsi.

## 2 HOW DO WE COLLECT YOUR PERSONAL DATA?

### TUNAKUSANYAJE TAARIFA ZAKO BINAFSI?

Your personal data is (a) provided by you; and/or (b) created by us during your engagement with us.

Taarifa zako binafsi (a) hutolewa na wewe mwenyewe; na (b) sisi huziandaa kutokana na maelezo yako wakati wa mazungumzo yetu na wewe.

## 3 THE TYPES OF PERSONAL DATA WE COLLECT FOR OUR PURPOSES AND THE APPLICABLE LEGAL BASIS FOR OUR DATA PROCESSING

### AINA YA TAARIFA BINAFSI TUNAZOZIKUSANYA KWA MATUMIZI YETU PAMOJA NA MSINGI WA KISHERIA UNAOTUMIKA KATIKA UCHAKATAJI WETU WA TAARIFA

In the context of your use of the Kijani App, we collect, store, and use personal data about you as set out in the 'personal data' column below. You will also find below the purpose of the processing and the legal basis we rely on for each type of personal data that we process about you.

Katika muktadha wa matumizi yako ya Aplikesheni ya Kijani, tunakusanya, tunahifadhi, na tunatumia taarifa zako binafsi kwa mpangilio kama ilivyo katika kipengele cha 'taarifa binafsi' hapa chini. Pia, hapa chini utaona lengo la uchakataji na msingi wa kisheria tunaoutumia kwa kila aina ya taarifa binafsi tunayoichakata kuhusu wewe.

If you fail to provide certain personal data when requested, we may not be able to perform all our legal and contractual obligations or carry out certain activities.

Kama utashindwa kutoa taarifa fulani inayokuhusu wewe unapoombwa, tunaweza kushindwa kutekeleza wajibu wetu wa kisheria na matakwa ya kimkataba au tutashindwa kufanya shughuli fulani.

It is important that the personal data we hold about you is accurate and up to date. Please keep us informed if your personal data changes during your use of the Kijani App.

Ni muhimu sisi kuwa na taarifa zako binafsi zilizo sahihi na zilizosasishwa. Tafadhali, tujulishe ikiwa taarifa zako binafsi zitabadirika wakati unapoendelea kutumia Aplikesheni ya Kijani.

| Personal data | Purpose | Legal basis |
| --- | --- | --- |
| **Data related to the use of the Kijani App,** such as:<br><br>**Taarifa zinazohusiana na matumizi ya Aplikesheni ya Kijani,** kama vile:<br><br>• Farming activity<br>Shughuli ya shambani<br>• Online activity in the Kijani App (such as the selected course by you).<br><br>Shughuli za mtandaoni katika Aplikesheni ya Kijani (kama vile somo ulilochagua) | Facilitating the Kijani App, including maintaining and ensuring a secured online environment on our Kijani App and providing (i) personalized advice on regreening methods and (ii) suggestions for different courses available in the Kijani App.<br><br>Anonymization of the data.<br><br>Kuiwezesha Aplikesheni ya Kijani, ikiwa ni | Necessary for the purpose of our legitimate interests to provide the Kijani App to you, including suggestions for different services (e.g. courses), and to maintain and improve the Kijani App.<br><br>Ni muhimu kwa madhumuni ya maslahi yetu halali ya kutoa Aplikesheni ya Kijani, pamoja na ushauri katika huduma tofautitofauti (mfano, masomo), na kuendeleza na kuboresha Aplikesheni ya Kijani.<br><br>Necessary for the purpose of our legitimate interest, |

| Personal data | Purpose | Legal basis |
|---|---|---|
| | pamoja na kudumisha na kuhakikisha mazingira salama mtandaoni katika Aplikesheni yetu ya Kijani na kutoa:<br><br>(i) Ushauri binafsi kuhusu mbinu za ukijanishaji<br><br>(ii) Ushauri kuhusu masomo tofautitofauti unapatikana katika Aplikesheni ya Kijani.<br><br>Ufichaji wa utambulisho wa taarifa. | namely, to maintain a secure online environment on our application<br><br>Ni muhimu kwa madhumuni ya maslahi yetu halali kama vile kudumisha mazingira salama mtandaoni katika aplikesheni yetu. |
| **Account data**, such as:<br><br>**Taarifa za akaunti,** kama vile:<br><br>● Username<br>Jina la mtumiaji<br>● Telephone number<br>Namba ya simu<br>● (GPS) location of the farm<br>Mahali shamba lilipo (GPS)<br>● User content (such as profile photo, photos of the progress, data uploads of the farm and the progress of the course you are doing, short story or bio (such as age, hobby, family situation etc. only if uploaded by user), comments and other materials (if uploaded by user)).<br><br>Maudhui ya mtumiaji (kama vile picha ya wasifu, picha za maendeleo, upakiaji wa taarifa za shamba na maendeleo ya somo unalojifunza, hadithi fupi au wasifu (kama vile umri, kitu unachopenda zaidi, hali ya kifamilia n.k. ikiwa vitapakiwa | Keep and maintain an accurate and adequate profile administration.<br><br>Tunza na dumisha matumizi sahihi na ya kutosha ya wasifu.<br><br>For general use of the Kijani App.<br><br>Kwa matumizi ya jumla ya Aplikesheni ya Kijani.<br><br>User content: customizing your Kijani App experience to your preferences and provided information.<br><br>Maudhui ya mtumiaji:<br><br>Pangilia mwonekano wa aplikesheni yako ya Kijanisha kadiri unavyopenda, kulingana na taarifa zilizopo. | Necessary for the purpose of our contractual relationship with you.<br><br>Ni muhimu kwa madhumuni ya mahusiano ya kimkataba kati yetu na wewe.<br><br>Necessary for the purpose of our legitimate interests to maintain an adequate profile administration.<br><br>Ni muhimu kwa madhumuni ya maslahi yetu halali katika kudumisha usimamizi madhubuti wa wasifu. |

| Personal data | Purpose | Legal basis |
|---|---|---|
| na mtumiaji), maoni na vitu vingine (kama vitapakiwa na mtumiaji) | Anonymization of the data.<br><br>Ufichaji wa utambulisho wa taarifa. | |

## 4 HOW LONG DO WE RETAIN YOUR PERSONAL DATA?

### JE, TAARIFA ZAKO BINAFSI TUNAZIHIFADHI KWA MUDA GANI?

We do not process your personal data any longer than necessary for the processing purpose.

Hatuchakati taarifa zako binafsi kwa muda mrefu kuliko inavyohitajika kulingana na madhumuni ya uchakataji.

In this context we keep your personal data for as long as your account on the Kijani App is active. Your personal data is deleted five years after the last activity on the Kijani App, or directly after deleting your account on the Kijani App.

Katika muktadha huu tunahifadhi taarifa zako binafsi kwa muda mrefu kadiri ya uhai wa akaunti yako katika Aplikesheni ya Kijani. Taarifa zako binafsi zitafutwa miaka mitano baadaye, tangu akaunti yako ilipotumika kwa mara ya mwisho katika Aplikesheni ya Kijani, au zitafutwa moja kwa moja baada ya wewe kufuta akaunti yako katika Aplikesheni ya Kijani.

If we are subject to a statutory retention period, we will retain your personal data for the period specified by the law.

Ikiwa tuko chini ya kipindi maalumu cha kisheria cha uhifadhi wa taarifa, tutahifadhi taarifa zako binafsi kwa muda uliowekwa kisheria.

Notwithstanding the above, we may retain your personal data for the length of any applicable limitation period for claims that might be brought against us later.

Hata hivyo, tunaweza kuhifadhi taarifa zako binafsi kwa muda mrefu zaidi kwa ajili ya madai ambayo yanaweza kuletwa dhidi yetu hapo baadaye.

In some circumstances, we may anonymize your personal data so that it can no longer be associated with you, in which case we may use such data without further notice to you.

Wakati mwingine, tunaweza kuficha utambulisho wa taarifa zako binafsi ili zisihusiane na wewe tena, katika mazingira hayo tunaweza kutumia taarifa hizo pasipo kukujulisha.

## 5 WITH WHOM WE SHARE THE PERSONAL DATA?

### JE, TAARIFA ZAKO BINAFSI TUNAZITUMIA NA NANI?

Where this is necessary in relation to the Kijani App, we will share your data with external service providers on the instructions and under the responsibility of Justdiggit. Such service providers are

considered “processors” under the GDPR. Your personal data will remain under Justdiggit’s control in such cases. These external service providers will always be subject to Justdiggit’s written instructions, including certain security obligations. We share your data with the following categories of processors:

Ikiwa hii ni muhimu katika Aplikesheni ya Kijani, tutawapa taarifa zako watoa huduma wengine kwa maelekezo na chini ya uangalizi wa Justdiggit. Watoa huduma hao wanachukuliwa kama “wachakataji” chini ya GDPR. Katika mazingira hayo, taarifa zako binafsi zitabaki chini ya udhibiti wa Justdiggit. Watoa huduma hao wakati wote watazingatia maelekezo ya kimaandishi ya Justdiggit, ikiwa ni pamoja na wajibu wa kiusalama. Taarifa zako tunazitumia na wachakataji walio katika makundi yafuatayo:

| Party<br><br>Mshirika | Purpose<br><br>Lengo |
|---|---|
| **Microsoft Azure** | **To host the Kijani App.**<br><br>**Kuendesha Aplikesheni ya Kijani** |
| **Google Analytics** | **To analyze and improve the use of the Kijani App.**<br><br>**Kutathmini na kuboresha matumizi ya Aplikesheni ya Kijani** |

Further, we may disclose or share your personal data:

Pia, tunaweza kutoa au kusambaza taarifa zako binafsi:

- to our group entities for business purposes, including administrative, management and accounting purposes, and as part of our regular reporting activities on company performance, in the context of a business reorganization or group restructuring exercise, for system maintenance support and hosting of data;

  katika makundi yetu kwa madhumuni ya kibiashara, kama vile kiutawala, kiusimamizi na madhumuni ya kiuhasibu, na ikiwa ni sehemu ya shughuli za kawaida za utoaji wa ripoti za utendaji kazi wa kampuni, katika muktadha wa kuboresha biashara au zoezi la urekebishaji wa kundi, kwa ajili ya kusaidia matengenezo ya mfumo na utunzaji wa taarifa.

- if we sell our company or part thereof (including separate assets), or if we merge with another company. In such event, we may share your personal data with the new owner or merging party respectively, but only to the extent necessary for the purpose for which your personal data are processed;

  kama tunauza kampuni letu au sehemu yake (ikiwa ni pamoja na mali tofauti), au kama tutaungana na kampuni nyingine. Katika mazingira hayo, tunaweza kutumia taarifa zako na mmiliki mpya au yeyote tuliyeungana naye, lakini ni kwa kiasi ambacho kinahitajika kulingana na madhumuni ya uchakataji wa taarifa zako binafsi.

- if we are subject to insolvency proceedings, as part of the sale of our assets by a liquidator (or similar); or

ikiwa tutakabiliwa na kesi za ufilisi, kama sehemu ya uuzaji wa mali zetu na mfilisi (au anayefanana naye); au

- we are legally obliged or allowed to do so. In such an event we shall share your personal data with the relevant supervisory authority, investigative authority or other governmental body.

  tunalazimika au tunaruhusiwa kisheria kufanya hivyo. Katika mazingira kama hayo, tutaipa taarifa zako binafsi mamlaka husika ya usimamizi au chombo kingine cha serikali.

## 6 WHERE DO WE STORE YOUR PERSONAL DATA?

### JE, TAARIFA ZAKO BINAFSI TUNAZIHIFADHI WAPI?

Justdiggit stores your personal data on servers located within the European Economic Area (EEA).

Justdiggit inahifadhi taarifa zako binafsi katika kanzidata zilizopo ndani ya Eneo la Kiuchumi la Ulaya (EEA).

## 7 YOUR RIGHTS

### HAKI ZAKO

In accordance with the applicable laws in the European Union, you have the right of access, the right to rectification, the right to erasure, the right to restriction of processing, the right to data portability and the right to object. Please note that most of these rights are not absolute and subject to exemptions in the law, and may only apply to certain types of personal data or processing.

Kwa mujibu wa sheria zinazotumika katika Umoja wa Ulaya, una haki ya kupata, haki ya kurekebisha, haki ya kufuta, haki ya kuzuia uchakataji, haki ya kuhamisha pamoja na haki ya kupinga. Kumbuka kwamba, haki nyingi zilizotajwa hapa si kamilifu na ziko chini ya misamaha ya kisheria, na zinaweza kutumika kwa aina fulani tu ya taarifa binafsi au uchakataji.

Below we set out your rights in more detail and give personal data on how you can exercise your rights.

Hapa tunaeleza kwa undani zaidi kuhusu haki zako na kutoa taarifa binafsi namna unavyoweza kutumia haki zako

We will respond to your request within one month, but have the right to extend this period to two months. If we extend the response period, we will let you know within one month from your request.

Tutajibu ombi lako ndani ya mwezi mmoja, lakini tuna haki ya kuongeza muda huo mpaka miezi miwili. Kama tutaongeza kipindi cha majibu, tutakujulisha ndani ya mwezi mmoja kuanzia ulipotuma maombi.

- *Access*: you are entitled to ask us if we are processing your personal data and, if we are, you can request access to your personal data (commonly known as a "data subject access request"). This enables you to receive a copy of the personal data we hold about you and to check that we are lawfully processing it. If your request is clearly unfounded or excessive, we reserve the right to charge a reasonable fee or refuse to comply in such circumstances.

*Kupata*: una haki ya kutuuliza kama tunachakata taarifa zako binafsi na, ikiwa tunachakata, unaweza kuomba kuzipata taarifa zako (kwa kawaida hujulikana kama “ombi la kupata taarifa”). Hii inakuwezesha kupata nakala ya taarifa zako binafsi tulizonazo na kuhakikisha kwamba tunazichakata kisheria. Kama itadhihirika kuwa ombi lako halina msingi au limezidi, tunahifadhi haki ya kutoza ada inayofaa au kukataa kutekeleza katika muktadha huo.

- *Correction or updating*: you are entitled to request that any incomplete or inaccurate personal data we hold about you is corrected.

    *Kusahihisha au kusasisha*: una haki ya kuomba na kuhakikisha kwamba taarifa yoyote binafsi isiyo kamili au isiyo sahihi tuliyonayo kuhusu wewe ni sahihi.

- *Erasure (deletion)*: you are entitled to ask us to delete or remove personal data in certain circumstances. There are certain exceptions where we may refuse a request for erasure, for example, where the personal data is required for compliance with law or in connection with claims. When we need to rely on an exemption, we will inform you about this.

    *Kufuta:* katika muktadha fulani, una haki ya kutuomba tufute au tuondoe taarifa zako binafsi. Hata hivyo, tunaweza kukataa ombi lako la kufuta kulingana na mazingira, kwa mfano, wakati ambapo taarifa zako binafsi zinahitajika kwa mujibu wa sheria au kuhusiana na madai. Wakati tunapohitaji kutegemea msamaha, tutakujulisha.

- *Restriction*: you are entitled to ask us to suspend the processing of certain of your personal data about you, for example if you want us to establish its accuracy or the reason for processing it.

    *Kuzuia:* una haki ya kutuomba kusitisha uchakataji wa taarifa fulani miongoni mwa taarifa zako binafsi, kwa mfano, ikiwa unataka tuzingatie usahihi wake au tutoe sababu ya kuichakata.

- *Transfer (data portability):* you may request the transfer of a copy of certain of your personal data to another party (if technically feasible). You have the right to ask that we provide your personal data in an easily readable format to another company. Please note, this right applies to the personal data you have provided to us and only if we use your personal data on the basis of consent or where we used your personal data to perform a contract with you.

    *Kuhamisha:* unaweza kuomba uhamisho wa nakala ya taarifa zako binafsi kwenda kwa mshirika mwingine (kama inawezekana kitaalamu). Una haki ya kutuomba tutoe taarifa zako binafsi katika mtindo unaosomeka kwa urahisi kwa kampuni nyingine. Kumbuka kwamba, haki hii inatumika katika taarifa binafsi ulizotupa na ikiwa tutatumia taarifa zako binafsi kwa msingi wa idhini au ambapo tulitumia taarifa zako binafsi kuingia mkataba na wewe.

- *Objection*: where we are processing your personal data based on a legitimate interest, you may object to processing on this ground. You also have a right to object where we are processing your personal data for the purposes of profiling. However, we may be entitled to continue processing your personal data based on our legitimate interests.

    *Kuzuia/Kupinga:* wakati tunachakata taarifa zako binafsi kulingana na maslahi halali, utaweza kupinga uchakataji kufanyika. Vilevile, una haki ya kupinga wakati tunachakata taarifa zako binafsi kwa lengo la kupata maelezo mafupi. Ingawa, tunaweza kuwa na haki ya kuendelea na uchakataji wa taarifa zako binafsi kwa msingi wa maslahi yetu halali.

- *Withdraw your consent:* Where you have provided your consent to our processing of your personal data you can withdraw your consent at any time. If you do withdraw consent, it will not affect the lawfulness of what we have done with your personal data before you withdrew consent.

  *Kuondoa idhini yako:* wakati ambapo umetoa idhini ya kuturuhusu kuchakata taarifa zako binafsi, pia unaweza kuondoa idhini hiyo wakati wowote. Ikiwa utaondoa idhini hiyo, bado haitaathiri uhalali wa tuliyoyafanya kwa kutumia taarifa zako binafsi kabla ya kuondoa idhini husika.

If you want to exercise any of these rights, or to withdraw your consent, please contact us in writing at info@justdiggit.org.

Kama unataka kutumia mojawapo ya haki hizi, au kuondoa idhini yako, tafadhali wasiliana nasi kwa maandishi kupitia baruapepe info@justdigit.org.

## 8 Right to lodge a complaint

### HAKI YA KUWASILISHA MALALAMIKO

You also have a right to lodge a complaint with a supervisory authority, in particular in the Member State in the European Union where you are habitually resident, where you work or where an alleged infringement of data protection law has taken place. A list of EU supervisory authorities and their contact details is available here.

Pia, una haki ya kuwasilisha malalamiko katika mamlaka ya usimamizi, hususan katika nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya ambapo wewe ni raia wake, ambapo unafanya kazi au mahali ambapo madai ya ukiukaji wa sheria ya ulinzi wa taarifa yamewasilishwa. Orodha ya mamlaka za usimamizi zilizopo katika Umoja wa Ulaya pamoja na mawasiliano yake, vinapatikana hapa.

In the Netherlands you can make a complaint to the *Autoriteit Persoonsgegevens* (tel. +31 70 888 8500 or at https://autoriteitpersoonsgegevens.nl/en).

Nchini Uholanzi, unaweza kuwasilisha malalamiko katika *Autoriteit Persoonsgegevens* (simu. +31 70 888 8500 au kupitia https://autoriteitpersoonsgegevens.nl/en).

## 9 Changes to this Privacy Notice

### MABADILIKO YA TAARIFA YA FARAGHA

This Privacy Notice will be changed from time to time.

Taarifa hii ya faragha itabadilishwa kulingana na wakati.

We may change this Privacy Notice from time to time. At all times, we will publish the up-to-date version in the Kijani App. If we make any important changes to this Privacy Notice (e.g. regarding the personal data we collect, how we use it or why we use it), we will notify you.

Tunaweza kubadilisha taarifa hii ya faragha kadiri muda unavyoenda. Wakati wote, tutachapisha toleo lililosasishwa katika Aplikesheni ya Kijani. Ikiwa tutafanya mabadiliko yoyote muhimu katika

taarifa hii ya faragha (mfano, kuhusu taarifa binafsi tunazozikusanya, namna tunavyozitumia au kwa nini tunazitumia), tutakujulisha.